# HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI
# SHULE YA SEKONDARI ITIGI

Mkuu wa shule+**255756658415/+255673988415**
M/Mkuu wa shule+**255766453072**
Patron:**+255769075278**

S.L.P.10,
**ITIGI.**

Kumb.Na*ITG/SS/KJ/KDTV/2024* Tarehe17/04/2024.

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi…………………………
S.L.P……………………………………
……………………………………

Yah:**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ITIGI HALMSHAURI YA ITIGI MKOA WA SINGIDA MWAKA 2024**

## 1.0UTANGULIZI:

Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano mwaka wa masomo 2024/2025 katika shule hii kwa tahasusi ya **HGL/HGK/HGFa/HGLi**

Shule ipo Mkoa wa Singida Halmashauri ya Itigi, ipo umbali wa Kilomita 1 (moja) kutoka makao makuu ya mji wa Itigi. Waweza kufika shuleni kwa usafiri wa reli ya kati au basi.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **01/07/2024** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **01/07/2024.** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **14/07/2024** saa 11:30 jioni.

## 2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia:-

## 2.1 Sare ya Shule

(a) Sare ya shule ni suruali **2** rangi ya **dark blue** kitambaa **suit material (estim)** Suruali iwe na **tanapuchini**, **linda2** na chini iwe na upana wa sentimeta 16 (mzunguko32cm) isiwe ya kubana
(b) Shati **2** rangi nyeupe mikono mirefu
(c) Tai ya dark blue yenye strips (mistari) nyeupe aje nayo (au anaweza kupata shuleni kwa Tsh.5,000/=)
(d) Viatu vya shule jozi mbili rangi **nyeusi** vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
(e) Soksi nyeusi jozi mbili (2)
(f) Sweta rangi ya dark blue shingo ya " V" aje nalo (au anaweza kupata shuleni kwa Tsh.18,000/=)
(g) Mkanda **mweusi wa ngozi** wa kuvalia suruali usiwe na mapambo
(h) Nguo za kushindia (shamba dress) ni suruali rangi ya **kaki** kitambaa suit **material** na track suit rangi nyekundu yenye michirizi (strips) myeupe.
(i) Sare ya michezo ni jezi moja nyekundu (**isiyo na maandishi wala nembo yoyote**) na bukta ya bluu moja.

(j) T-shirt rangi ya **dark blue** yenye kola (form six) aje nayo (au anaweza kupata shuleni kwa Tshs.15,000/=
(k) Viatu vya michezo ni vya rangi yoyote
**NB:Hairuhusiwi mwanafunzi kuja na nguo za nyumbani.`**

### 2.2 Michango ya Shule

**Michango inayolipwa na mwanafunzi kwa mwakani:-**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha zote zilipwe kwenye Akaunti Na. ***50701100052*– ITIGI SECONDARY SCHOOL RECCURENT** benki ya NMB, **hakikisha mwanafunzi anakuja na Bank Pay in slip** iliyo andikwa jina la mwanafunzi na siyo la mtu mwingine, **Mfano Samwel Ally Mbogo – Kidato cha Tano** (fedha tasilimu hazipokelewi)

### 2.3 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

(i) Kila mwanafunzi mwenye Bima ya Afya ya NHIF anatakiwa kuja nayo au aje naTsh. 52,000/= kwa ajili ya matibabu/kupatiwa bima ya NHIF (**hii ni lazima kwa wanafunzi wote**). Mwanafunzi mwenye miaka 18 au zaidi lazima aje na na mbaya NIDA kwa ajili ya bima na matumi zimbalimbali.
(ii) Daftari kubwa saba(7)aina ya counter book3Q
(iii) Ream 2 za karatasi aina ya **A4** kwa mwaka
(iv) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (HGL/HGK/HGFa/HGLi)
(v) Scientific calculator
(vi) Godoro (2½ kwa 6) ajenalo
(vii) Mashuka pair 2 rangi ya bluu bahari, blanket 1, foronya 1 na Chandarua 1(2½ kwa 6)
(viii) Vyombo vya chakula ambavyo ni sahani, bakuli, kijiko na kikombe (vya aluminium)
(ix) Ndoo 2 ndogo zenye mifuniko (ujazo wa litakumi)
(x) Mfagio laini 1 (soft brooms), squizer 1, Mfagio wa nje 1 (chelewa)
(xi) Dawa/sabuni ya kusafishia (ainaya Careline, MCL au Dex) lita tano (5) kwa ajili ya usafi
(xii) **HGL na** walete reki 1
(xiii) **HGK** walete jembe 1 jipya na mpini wake,
(xiv) **HGFa na HGLi** walete kwanja 1 na hard broom 1,
(xv) Nguo za ndani za kutosha
(xvi) Galoni la ujazo wa Lita tano (5) kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa

## 3.0 SHERIA MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 nakama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi nauendeshaji wa Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku( Preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule.
x. Nimarufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Mwanafunzi ataruhusiwa kutoka nje ya shule akiwa amevaa sare rasmi ya shule (suruali ya dark blue na shati nyeupe au tisheti yenye nembo ya shule) tu.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu au kifaa cha simu shuleni (charger, line, ear phones, usb cables n.k) kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi. Mwanafunzi akikamatwa na simu au kifaa tajwa hapo juu adhabu yake ni mifuko kumi ya saruji na kufukuzwa shule.**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Nimarufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi**

**kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi haruhusiwi kusuka, kunyoa mitindo, kufuga ndevu wala kucha**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

- **Mzazi unashauriwa kumfungulia mwanao akaunti ya Benki yaNMB au CRDB ili kuepuka usumbufu (mzazi lazima umkabidhi mwanao kiasi cha fedha kwa ajili ya matumizi binafsi)**

## 3.1 MAKOSA YATAKAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI

a) Wizi.
b) Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa ya kulevya.
d) Makosa mengine ya jinai.
e) Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake au mtumishi.
f) Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine.
g) Kudharau bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Taifa, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
h) Kuoa au kuolewa.
i) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
j) Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
k) Kugoma, kufanyafujo, kushawishi, kuchochea na kuongoza migomo, au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni, kutoa lugha ya matusi kwa kiongozi wako au kwa mwanafunzi mwenzako.
l) Kukataa adhabu halali.
m) Kujiachisha shule mwenyewe.
n) Kumiliki au kutumia simu ndani ya eneo la shule (**mwanafunzi asije na simu shuleni**)
o) Kuchelewa kufika shuleni kwa muda halali uliopendekezwa na shule
p) Nimarufuku kutembelea nyumba za walimu bila ruhusa maalumu
q) Kutokuvaa sare elekezi ya shule, mfano viatu, suruali, Tisheti n.k
r) Kufuga ndevu, kusuka, au kuachia nywele ndefu kichwani.
s) Kuwa nje ya darasa wakati wa vipindi bila kibali.
t) Kutohudhuria vipindi vya usiku na asubuhi (night and morning preparation)
u) Kumgomea kiongozi halali aliyeteuliwa au kuthibitishwa na serikali kuu au Baraza la serikali ya wanafunzi kwa ajili ya kuongoza wanafunzi.
v) Kuwa nje ya eneo la shule baada ya saa 12:00 jioni
w) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

## 4.0 Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujona makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Mwanafunzi aje na Nakala (copy) ya CHETI CHA MATOKEO (**RESULTSLIP**) ya kidato cha nne na cheti cha kuzaliwa kwa ajili ya utambulishowake

**5.0** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**Karibu Sana Shule ya Sekondari Itigi**



JacobP.Mwabeza

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI ITIGI
S.L.P. 10
ITIGI

**MKUU WA SHULE**

**NB:Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simuna watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NIVEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WATAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-**

- **Mkuu wa shule +255 756 658 415**
- **Makamu Mkuu wa Shule +255 766 453 072**
- **Mwandamizi Taaluma +255 687 448 946**
- **Mwandamizi Malezi +255 717 953 734**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI

# SHULE YA SEKONDARI ITIGI

### KIAMBATANISHO A. FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ITIGI

### A. SEHEMU YA MWANAFUNZI

**MWANAFUNZI AJAZE SEHEMU HII**

1.Mimi------------------------------------------------------------ ninakubali kujiunga na Shule ya Sekondari Itigi kwa Tahasusi (combination) ya.................

2. Mimi nikiwa Mwanafunzi wa ITIGI Sekondari, ninakubali kwamba:

   a. Nitafika Shuleni siku ya kufungua na bila kuchelewa kila muhula
   b. Nitatii sharia zote za shule pamoja na kutoshiriki katika ulevi, migomo na migogoro ya aina yeyote.
   c. Sitaleta shuleni wala kuvaa mavazi yasiyo ya heshima k.m. nguo za kubana, kofia, miwani ya giza, pete za urembo.
   d. Nitatumia juhudi na maarifa yote kujiimarisha kitaaluma ikiwa ni pamoja na kuhudhuria vipindi na kufanya mazoezi na mitihani yote (k.v.usafi na elimu ya kujitegemea).

**SainiyaMwanafunzi---------------------------------Tarehe-------------------------------**

### B: SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

**MZAZI/MLEZI AJAZE SEHEMU HII**

1. Mimi....................................................... nimekubali mtoto wangu.......................................... ajiunge na Shule ya Sekondari ITIGI kuanzia tarehe..................................................

**Ninaahidi kwamba:**

a) Nitawasaidia walimu kumlea mwanangu kitaaluma nakitabia. Nitamuonya na kumsisitiza mwanangu kutii sharia zote za shule na kuishi maisha mazuri kwa maadili ya kiuanafunzi.
b) Nitamkataza kuvaa nguo zisizo za heshima k.m. nguo za kubana, kofia, miwani ya giza n.k.
c) Nitampatia motto wangu nauli ya kuja shuleni na kurudi likizo bila kuchelewa.
d) Nitahakikisha anakuja shuleni siku ya kufungua kila muhula bila kuchelewa.

2. Anwani yangu ya kudumu
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................

Sahihi ya Mzazi/Mlezi---------------------------------------------Tarehe ----------------------------------(Tafadhali njoo na fomu hii unapokuja shuleni ikiwa imejazwa).

## HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI

# SHULE YA SEKONDARI ITIGI

Sim... hule 0756658415/0673988415 ...),

MakamuM/Shule 0766453072 ITIGI


### FOMU YA MAELEZO BAYANA (PERSONAL PARTICULARS) KWA AJILI YA USAJILI

### IJAZWE NA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la mwanafunzi kama alivyojiandikisha kwenye mtihani wa Kidato cha Nne..........................................................................................

2. Jina kamili la Baba/Mlezi.......................................................

(a)Anwani ya Baba/Mlezi.....................................................

(b)Namba ya simu ya Baba/Mlezi......................................................

(c)Nyumbani ........................ Mtaa/Kijiji........................... Kata..................

Tarafa................................Wilaya.............................................anakokaa.

3.Jina la Mama/Mlezi.......................................................

(a)Anwani ya Mama/Mlezi......................................................

(b) Namba ya simu ya Mama/Mlezi......................................................

(c)Nyumbani...............................Mtaa/Kijiji.................... Kata..........................

Tarafa..........................Wilaya.................................... anakokaa.

4. Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi...........................

5.Mahalia lipozaliwa...........................Mkoa.................Wilaya..........................
Kijiji/Mtaa...........................

6.Kazi ya Baba/Mlezi...........................

7.Kazi ya Mama/Mlezi...........................

8. Je mwanafunzi anachokilema chochote?............................Kijaze (kama kipo) .......................

9. Taja ndugu watatu ambao wanaweza kufika shuleni na kutoa msaada kwa mwanao

| SN | JINA | KAZI | UHUSIANO | NA.YASIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |

Saini ya Mzazi/Mlezi:..........................................................

TAREHE............................................................

HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI

SHULE YA SEKONDARI ITIGI

Simu:Mkuu wa Shule 0756658415/0673988415 S.L.P.10,
MakamuM/Shule 0766453072 ITIGI

## MEDICAL EXAMINATION FORM

Date……………………

To the Medical Officer

…………………………………………

…………………………………………

Dear Sir/Madam

REF: **REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine Mr. /Miss…………………………………………… as to his/ her fitness as a full time student of Itigi Secondary School. May I kindly ask you to fill in the particulars given in the form hereunder.

YoursSincerely

JacobP.Mwabeza
**HEADMASTER**

THE HEADMASTER
ITIGI SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 10
ITIGI

### TOBE COMPLETEDBYTHEMEDICAL OFFICER

1. Bloodcount(White Blood cells)……………………………………
2. Stool examination……………………………………………
3. Urine Examination……………………………………………
4. Gestation (for girls only)……………………………………
5. Veneral disease……………………………………………
6. T.BTest……………………………………………………
7. E.N.TProblems…………………………………………………
8. Defects of (a)The left and right eye………………………………
   (b)The chest……………………………………………
9. Any CHRONIC or FAMILY diseases e.g. Epilepsy, Sickle cell etc.
   ……………………………………………………………………………

### DECLERATION

I have examined Mr/Miss ........................................................................and certify that he/she is Physically fit/unfit to pursue his/her studies as stated above.

…………………………
**Name of Medical Officer**

…………………
**Signature of Medical Officer**

**Designation……………………**

**Official Stamp……………………**

**Orodha ya baadhi ya Vitabu**

**Mzazi unaweza kumnunulia mwanao vitabu vifuatavyo kulingana na tahasusi aliyopangiwa**

| Na. | Somo | Juna la Kitabu |
|---|---|---|
| 1 | GEOGRAPHY | a) Human and Economic Geography Advanced level D.T.Msabila.<br>b) Practical Geography Advanced Level (Map Reading Photography Interpretation Field Research, Statistics & Introduction to Survey)<br>c) Landforms in Africa: An introduction to Geomorphology– Colin Buckle<br>d) Practical Geography for Africa – John Pritchard<br>e) Geography: An Integrated Approach– David Waugh<br>f) Physical Geography for Secondary Schools– D.T.Msabila<br>g) Physical Geography of Africa with Diagrams– Burnett<br>h) Principles of Physical Geography– Monk House<br>(Vitabu vya T.I.E vya Geography) |
| 2 | HISTORY | a) History for Secondary Schools Form Five– T.I.E (2016)<br>b) History for Secondary Schools Form Six– T.I.E(2016)<br>c) Contemporary Historical Events Advanced Level History One Tumaini, S.C.K (2010).<br>d) Essentials in Advanced Level History Paper2,Yassin,S.<br>e) History of Modern Europe in the 19$^{th}$Century– P.Cock<br>f) History Paper Two– Lesson Notes– Bakari Madaya<br>g) History paper One– Lesson Notes– Bakari Madaya<br>(vinapatikana shuleni) |
| 3 | GENERAL STUDIES | a)General Studies for Advanced Level Certificate Form Five R.F.Mbalase.<br>b)General Studies, Supplimentary Book for Advanced Level and Colleges,-Konrad Adenaker Stiftung, 2$^{nd}$Edition |
| 4 | KISWAHILI | a) Kiswahili Kidato cha Tano– T.I.E<br>b) Kiswahili Kidato cha Sita– T.I.E<br>c) Nadharia ya Fasihi kidato cha Tano na Sita – Nyambari Nyangwine<br>d) Nadharia ya Lugha Kidato cha Tano na Sita– T.I.E<br><br>**RIWAYA**<br>a) Usiku Utakapokwisha<br>b) VutaN' kuvute<br>c) Mfadhili<br>d) Kufikirika<br><br>**TAMTHILIYA**<br>a) Morani<br>b) KivuliKinachoishi<br>c) Kwenye Ukingo wa Thim<br>d) Nguzo Mama |

| | | |
|---|---|---|
| | | □**USHAIRI**<br>i. Kimbunga<br>ii. Fungate ya Uhuru .<br>iii. MapenziBora |
| 5 | ENGLISHLA NGUAGE | **ENGLISHLANGUAGEI**<br>a) English for Advanced Leveles Phonology and Stylistics<br>b) Advanced English Language I– Shadrack Ndambo<br>c) Advanced Level English Language– Nicholous Asheri<br>d) Advanced English Language– Oxford<br><br>**ENGLISHLANGUAGEII**<br>Advanced level Literature Analysis<br>• **NOVEL**<br>i. A man of the people<br>ii. The Beautiful ones are not yet born<br>iii. His excellent the head of state<br><br>• **PLAYS**<br>i. An enemy of the people<br>ii. Betrayal in the city<br>iii. I will marry when I want<br>iv. Lwandamagere<br><br>• **POETRY**<br>i. Selected poems<br>ii. The wonderful surgeon |